

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



MASHARTI YA MKOPO KWA WANAWAKE NA VIJANA

1. Ofisi ya Maendeleo ya Jamii Jiji itaandaa majina ya wakopaji chini ya usimamizi wa Mratibu wa Mikopo ya Jiji.
2. Ofisi ya Maendeleo ya Jamii Jiji itaandaa rejesta ambayo itaonyesha:-
 - Jina la Wakopaji
 - Anuani ya Wakopaji
 - Jinsi za wahusika
 - Aina ya Kikundi, Saccos na Vicoba
 - Kiasi cha fedha kinachoombwa
 - Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa
3. Wakopaji wataingia Mkataba na Ofisi ya Halmashauri ya Jiji kwa kusaini fomu ya Mkataba baada ya Kamati ya mfuko ya Halmashauri kuridhia.
4. Mkopaji atalazimika kuhudhuria mafunzo ya ujasiriamali, uongozi na uendeshaji miradi.
5. Mkopaji atakayechelewesha kulipa deni katika muda muafaka atatozwa riba ya asilimia 20% badala ya asilimia 10%.
6. Riba ya Mkopo ni asilimia 10%.
7. Muda wa kusubiri (Grace Period) msamaha baada ya kupokea mkopo ni mwezi mmoja na itategemea na aina ya mradi.
8. Mkopo utakaotolewa na mfuko huu utanzia shilingi laki tano hadi milioni tatu (500,000/= - 3,000,000/=) kwa kikundi cha Saccos na Vicoba.
9. Waombaji watakaokopeshwa ni wale walio katika:-
 - Kikundi ambacho kinatambulika na Ofisi ya Kata na kimesajiliwa.
 - Saccos.
 - Vikoba inayotambuliwa na Ofisi ya Kata.
10. Muda wa urejeshaji mkopo huu ni kuanzia miezi miwili (2) hadi mwaka mmoja (1).
11. Kamati ya mkopo ya Jiji itafanya ufuatiliaji na kutoa ushauri.
12. Mkopaji lazima awe Mkazi wa eneo husika.
13. Mkopo huu utakuwa ni wa mzunguko na unatakiwa kurejeshwa ili na wengine wakope (Revolving Fund) Asilimia mbili (2%) ya riba itaingia katika mfuko moja kwa moja.
14. Asilimia tano (5%) ya riba na Ofisi ya Mratibu wa mfuko wa Halmashauri kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya mikopo
15. Mkopo huu utarejeshwa kwa wakopaji kulipia Benki moja kwa moja kupitia Benki ya **CRDB** Akaunti ya **HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM A/C NO. 015021142000** Tawi la **AZIKIWE PREMIER.**